HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 28/04/2022 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA SOKO KUU LA CHIFU KINGALU.

Wajumbe waliohudhuria:

1.	Mhe. Pascal M. Kihanga	__	Mstahiki Meya – Mwenyekiti
2.	Ndg. Ally H. Machela	__	Mkurugenzi wa Manispaa -Katibu
3.	Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele	__	Naibu Meya - Mjumbe
4.	Mhe. Abdallah Ally Meya	__	Mjumbe
5.	Mhe. Hadija Kombo Kibati	__	Mjumbe
6.	Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani	__	Mjumbe
7.	Mhe. Melchior Peter Mwamnyanyi	__	Mjumbe
8.	Mhe. Abdallah Mohamed Chamgulu	__	Mjumbe
9.	Mhe. Zamoyoni Juma Abdallah	__	Mjumbe
10.	Mhe. Salum Mrisho Chunga	__	Mjumbe
11.	Mhe. Amina Hussein Zihuye	__	Mjumbe
12.	Mhe. Peter Joel Dhahabu	__	Mjumbe
13.	Mhe. Latifa Saidi Ganzel	__	Mjumbe
14.	Mhe. Samuel Alfred Msuya	__	Mjumbe
15.	Mhe. Eng. Hamisi Hamadi Ndwata	__	Mjumbe
16.	Mhe. Warda Omari Bazia	__	Mjumbe
17.	Mhe. Amini Abdallah Tunda	__	Mjumbe
18.	Mhe. Hamisi Ally Kilongo	__	Mjumbe
19.	Mhe. Athumani Omary Lujuo	__	Mjumbe
20.	Mhe. Ally Rashid Kalungwana	__	Mjumbe
21.	Mhe. Majuto Athumani Mbuguyu	__	Mjumbe
22.	Mhe. Rahma Lashayo Maumba	__	Mjumbe
23.	Mhe. Namala Johaness Mchunguzi	__	Mjumbe
24.	Mhe. Mwanaidi Ebrahim Ngulungu	__	Mjumbe
25.	Mhe. Salima Bonzo Mbandu	__	Mjumbe
26.	Mhe. Lt.Col(Mst) Ahmed S. Mazora	__	Mjumbe
27.	Mhe. Mch. Thomas Benedict Butabile	__	Mjumbe
28.	Mhe. Marco Mathias Kanga	__	Mjumbe
29.	Mhe. Emmy Kiula Rajabu	__	Mjumbe
30.	Mhe. Grace Luwis Mkumbae	__	Mjumbe
31.	Mhe. Zinduna Kombo Selemani	__	Mjumbe
32.	Mhe. Aisha Ahmad Kitime	__	Mjumbe
33.	Mhe. Joel Albert Kisome	__	Mjumbe
34.	Mhe. Zuberi George Mkalaboko	__	Mjumbe
35.	Mhe. Seif Zahoro Chomoka	__	Mjumbe
36.	Mhe. Rashid Ramadhani Matessa	__	Mjumbe

37.	Mhe. Selestini Savini Mbilinyi	__	Mjumbe
38.	Mhe. Juma Issa Kiduka	__	Mjumbe
39.	Mhe. Madaraka S. Bindyanguze	__	Mjumbe
40.	Mhe. Hassan M. Maringo	__	Mjumbe

Wajumbe wasiohudhuria kwa taarifa

1.	Mhe. Abdulaziz Mohamed (Mb)	__	Mjumbe
2.	Mhe. Dr. Christine G. Ishengoma (Mb)	__	Mjumbe
3.	Mhe. Norah Mzeru (Mb)	__	Mjumbe

Viongozi waalikwa waliohudhuria

1.	Mhe. Albert G. Msando	__	Mkuu wa Wilaya ya Morogoro
2.	Ndg. Erasto Gowele	__	Afisa Usalama Wilaya
3.	SP. Azizi A. Mshamu	__	Mkuu wa Polisi Wilaya
4.	Ndg. Festo Mkoma	__	Rep. MD – MORUWASA
5.	Eng. Erick Mtambi	__	Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya
6.	Ndg. Edina B. Oscar	__	Kaimu Katibu Tawala Mkoa Msaidizi Huduma za Serikali za Mitaa.
7.	Ndg. Erasmus Haule	__	Afisa Usalama
8.	Mhe. Chief Sylvester Yaredi	__	Katibu wa CCM Wilaya
9.	Mhe. Maulidi Chambilila	__	Katibu Mwenezi na siasa CCM Wilaya
10.	Ndg. Janeth Chatta	__	Kaimu Katibu Tawala Wilaya
11.	Mhe. Fikiri Juma	__	Mwenyekiti wa CCM Wilaya
12.	Eng. Leocard Sikambale	__	HOPLU - TANROADS
13.	Dr. David P. Rwegoshora	__	Kutoka TPSIS
14.	Ndg. Hassan M. Haji	__	Kutoka TPSIS
15.	Ndg. Christine D. Rwegoshora	__	Kutoka TPSIS
16.	Ndg. Ever F. Issaya	__	Kutoka TPSIS
17.	Ndg. Shaban R. Mtatura	__	Kutoka TPSIS
18.	Ndg. Shabani R. Mbiru	__	Kutoka TPSIS
19.	Ndg. Juma Hassan Mpando	__	Kutoka TPSIS
20.	Ndg. Simban A. Msakuzi	__	Kutoka TPSIS
21.	Ndg. Omary A. Betto	__	Kutoka TPSIS
22.	Ndg. Amina P. Maganga	__	Kutoka TPSIS
23.	Ndg. Emmanuel Edward Mwita	__	Kutoka TPSIS
24.	Ndg. Mbaraka S. Matete	__	Katibu wa Tiba asili Kata ya Kichangni.
25.	Ndg. Amina Kibela	__	Meneja wa Kanda ya Mashariki – NEMC
26.	Ndg. Joyce Omolo	__	Kutoka NEMC
27.	Ndg. Josiah Murunya	__	Kutoka NEMC

Wakuu wa Idara na Vitengo waliohudhuria;

1.	Ndg. Pilly Kitwana	__	Afisa Utumishi wa Manispaa
2.	Ndg. Enedy Mwanakatwe	__	Afisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa
3.	Ndg. Samwel Subi	__	Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka ngumu wa Manispaa
4.	Ndg. Mwajuma Samgela	__	Kaimu Afisa Tarafa wa Manispaa
5.	Ndg. Epiphania Matafu	__	Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Manispaa
6.	Ndg. Evance Kutona	__	Afisa Usafirishaji wa Manispaa
7.	Ndg. Frank E. Mwago	__	Kaimu Afisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Manispaa
8.	Ndg. Upendo Elias	__	Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Manispaa
9.	Ndg. Festus Herman	__	Afisa Biashara wa Manispaa
10.	Ndg. Liston N. Mwalugula	__	Afisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa
11.	Ndg. Isaac Ashery	__	Kaimu Mweka Hazina wa Manispaa
12.	Ndg. Sophia Kingwahi	__	Afisa Utamaduni wa Manispaa
13.	Ndg. Neema Michael Dachi	__	Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa
14.	Ndg. Jafari A. Makupula	__	Afisa Ununuzi na Ugavi wa Manispaa
15.	Ndg. Elikarim S. Tyeah	__	Kaimu Mwanasheria wa Manispaa
16.	Ndg. Pendo Chagu	__	Afisa Uchaguzi wa Manispaa
17.	Ndg. D.P Mhaiki	__	Kaimu Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa
18.	Eng. Tedrous Michael	__	Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa Manisaa
19.	Ndg. Norbert Bilaba	__	Afisa Afya wa Manispaa
20.	Ndg. Feliciana Katemana	__	Mratibu wa TASAF wa Manispaa
21.	Dr. Charles Mkombachepa	__	Mganga Mkuu wa Afya wa Manispaa
22.	Ndg. Lusibilo Mwaisunga	__	Katibu TSC wa Manispaa
23.	Ndg. Chausiku Masegenya	__	Afisa Elimu Msingi wa Manispaa
24.	Ndg. Emeline Kihunrwa	__	Kaimu Afisa Mipangomiji, Ardhi na Maliasili wa Manispaa
25.	Ndg. Sylivia Kibiki	__	Kaimu Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji wa Manispaa
26.	Ndg. Alatutosia Y. Sanga	__	Afisa Masoko

Watendaji wa Kata waliohudhuria:-

1.	Ndg. Laurent Masanja	__	Mtendaji wa Kata ya Tungi
2.	Ndg. Christopher Libent	__	Kaimu Mtendaji wa Kata ya Mlimani
3.	Ndg. Hamisi Ally Ismail	__	Mtendaji wa Kata ya Mkundi
4.	Ndg. Michael A. Mgowe	__	Mtendaji wa Kata ya Lukobe
5.	Ndg. Andrew Edward Luka	__	Mtendaji wa Kata ya Mjimpya
6.	Ndg. Baraka Lemaha	__	Mtendaji wa Kata ya Mindu
7.	Ndg. Hadija K. Hamisi	__	Mtendaji wa Kata ya Mji Mkuu
8.	Ndg. Khalifa H. Mwakalinga	__	Kaimu Mtendaji wa Kata ya Chamwino
9.	Ndg. Witness Matowo	__	Mtendaji wa Kata ya Magadu
10.	Ndg. Helena Mgallah	__	Mtendaji wa Kata ya Bigwa
11.	Ndg. Josepher B. Kisaka	__	Mtendaji wa Kata ya Kihonda Maghorofani
12.	Ndg. Maria J. Shine	__	Mtendaji wa Kata ya Kingo
13.	Ndg. Mariam Khalid Ngoda	__	Mtendaji wa Kata ya Uwanja wa Taifa
14.	Ndg. Emiliana J. Mitula	__	Mtendaji wa Kata ya Mwembesongo
15.	Ndg. John Joseph	__	Mtendaji wa Kata ya Luhungo
16.	Ndg. Prisca Mawallah	__	Mtendaji wa Kata ya Boma
17.	Ndg. Masanja M. Nkinga	__	Mtendaji wa Kata ya Mazimbu
18.	Ndg. Nguya Ibrahim Rashid	__	Mtendaji wa Kata ya Kingolwira
19.	Ndg. Omary S. Samata	__	Kaimu Mtendaji wa Kata ya Kauzeni
20.	Ndg. Mwajabu R. Hassani	__	Mtendaji wa Kata ya Mafisa
21.	Ndg. Merina C. Singano	__	Mtendaji wa Kata ya Kichangani
22.	Ndg. Amina Said	__	Mtendaji wa Kata ya Mafiga
23.	Ndg. Hawa R. Uvilla	__	Kaimu Mtendaji wa Kata ya Sultan Area
24.	Ndg. Justa Medard	__	Mtendaji wa Kata ya Kilakala
25.	Ndg. Mariam S. Rajabu	__	Mtendaji wa Kata ya Mbuyuni
26.	Ndg. Fatma H. Mkwenda	__	Mtendaji wa Kata ya Sabasaba
27.	Ndg. Tatu H. Ally	__	Mtendaji wa Kata ya Kihonda
28.	Ndg. Christina Ngonyani	__	Mtendaji wa Kata ya Mzinga
29.	Ndg. Aziza Omari	__	Mtendaji wa Kata ya Kiwanja cha Ndege

Sekretarieti:-

1.	Ndg. Daudi A. Kibwana	__	Katibu wa Mikutano
2.	Ndg. Deogratias Butabile	__	Katibu wa Mikutano
3.	Ndg. Theresia Mbena	__	Katibu wa Mikutano
4.	Ndg. Jimmy Katabaruki	__	Katibu wa Mikutano
5.	Ndg. Mwasi Mulwambo	__	Katibu wa Mikutano
6.	Ndg. Lilian Lemunge	__	Katibu wa Mikutano
7.	Ndg. Lilian Henerico	__	Afisa Habari

HMM/BM/81/ 2021/2022 Kufungua Mkutano

Baada ya akidi kutimia Katibu alimkaribisha Mstahiki Meya (Mwenyekiti) ili afungue mkutano.

Kabla ya Mkutano kufunguliwa Mstahiki Meya aliwaongoza Wajumbe, Wataalam, Viongozi walioalikwa na Wananchi kwa ujumla kuimba wimbo wa Taifa na alisoma dua ya kuiombea Halmashauri.

Mstahiki Meya aliwakaribisha Wajumbe na wote waliohudhuria na alifungua Mkutano saa 5:25 asubuhi.

Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu) alitoa taarifa ya uwepo wa viongozi wa Kampuni binafsi ya Ulinzi na Usalama wa mali za Raia (Tanzania Private Security Integration Services) TPSIS na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Maizingira (NEMC) Kanda ya Mashariki ambao wote kwa pamoja wameomba kuja kutoa mada za kazi zao wanazotekeleza.

Kutokana na ufinyu wa muda, Mstahiki Meya aliwakaribisha wote na kuwaomba wajitambulishe kisha aliwaomba watafute siku nyingine kuja kutoa mada zao kwa Waheshimiwa Madiwani na Wataalamu wa Halmashauri.

Walijitambulisha kwa niaba ya wenzao kama ifuatavyo:-

1. Ndg. Amina Kibela – Kutoka NEMC Kanda ya Mashariki ambaye aliomba ushirikiano katika utunzaji wa Mazingira
2. Dr. David P. Rwegoshora - Kutoka Kampuni binafsi ya Ulinzi na Usalama wa Mali za Raia (TPSIS). Alieleza kuwa lengo la kuanzisha Kampuni hiyo ni kuhakikisha usalama wa mali za Raia unakuwepo.

Baada ya utambulisho huo, Mstahiki Meya aliwakaribisha Katibu wa Chama Cha Mapinduzi na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro ili waweze kuongea machache.

1. **Salamu za Katibu wa CCM Wilaya:-**
   Katibu wa CCM Wilaya aliwashukuru Wajumbe wa Baraza la Madiwani na Watendaji wa Halmashauri kwa kushirikiana kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025.

2. **Salamu za Mkuu wa Wilaya:-**
   Alianza kwa kuwasalimia wote waliohudhuria na kumshukuru Mstahiki Meya kwa kumwalika kuhudhuria Mkutano.

Aidha alitoa taarifa zifuatazo:-

i) Kuhusu kazi ya tathmini kwenye Mitaa mitatu katika Kata ya Mindu:-

Alieleza kuwa Mhe. Samia Suluhu Hassani – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza ifanyike tathmini kuhusu Wananchi wa Mtaa wa Mindu kama wanachafua na kuharibu Mazingira kwenye Bwawa la Mindu.

Mkuu wa Wilaya alieleza kuwa kazi hiyo imekamilika na aliiagiza Kamati ya Mipangomiji na Mazingira pamoja na Diwani wa Kata ya Mindu wafike ofisini kwake siku ya Ijumaa tarehe 29/04/2022 kupitia taarifa ya tathimini na wafanye ziara kwenda kujiridhisha kwenye eneo husika.

ii) Zoezi la kuandikisha Anwani za Makazi:-

Alitoa pongezi kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro kwa kukamilisha zoezi la kuandikisha Anwani za Makazi kwenye eneo la Utawala la Manispaa ya Morogoro. Aliagiza kuwa maeneo yaliyobaki ambayo hayakufikiwa yafikiwe.

iii) Maandalizi ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022:-

Aliagiza kuwa Kamati ya Fedha na Uongozi isimamie na kuratibu miradi yote itakayozinduliwa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2022 ili iweze kukamilika kulingana na thamani ya fedha zilizotolewa na Serikali.

iv) Kuhusu ukamilishaji wa miradi ya Maendeleo ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro:-

Alisisitiza kuwa miradi yote ya Halmashauri ambayo ina fedha itekelezwe na kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2021/2022.

v) Kuhusu mikataba ya Wafanyabiashara eneo la Zimamoto:-

Agizo

Aliagiza kuwa mikataba **51** ya Wafanyabiashara eneo la Zimamoto ambayo haipo rasmi ifutwe na kuingiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na kulipa Mapato ya Halmashauri.

vi) Kuhusu stendi ya Daladala Mafiga:-

Agizo

Aliagiza kuwa Stendi ya Daladala Mafiga ifanye kazi, magari yote yanayoenda Wilayani yaanzie hapo.

HMM/BM/82/2021/2022 Kuridhia Agenda za Mkutano

Wajumbe waliridhia agenda zifuatazo:-

1) Kufungua Mkutano
2) Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro.
3) Kusoma kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani
   - Tarehe 01/02/2022 (Taarifa za Kata).
   - Tarehe 03/02/2022 (Kawaida).
   - Tarehe 10/02/2022 (Mapitio ya bajeti 2020/2021).
   - Tarehe 10/02/2022 (Uwasilishwaji wa Bajeti ya mwaka 2022/2023).
   - Tarehe 10/02/2022 (Bajeti ya TARURA)
4) Yatokanayo na mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 03/02/2022 (kawaida) na tarehe 10/02/2022 (maalum bajeti)
5) Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo:-
   5.1 Kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022.
   5.2 Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022.
   5.3 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022.
   5.4 Kamati ya kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022.
   5.5 Kamati ya Maadili ya Madiwani kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022.
6) Mapitio ya Sheria Ndogo ya ada ya uzoaji wa taka ya mwaka 2019 pamoja na mapendekezo ya Sheria Ndogo ya usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa Morogoro ya mwaka 2022.
7) Taarifa ya Muundo wa mgawanyo wa majukumu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM).
8) Taarifa mbalimbali:
   a) Mapendekezo ya Wafanyakazi hodari wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa mwaka 2022.
   b) Taarifa ya mashauri ya nidhamu ya Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro
   c) Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Waheshimiwa Madiwani
   d) Taarifa ya Stendi ya Daladala Mafiga
9) Kufunga Mkutano.

HMM/BM/83/ 2021/2022 Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro

1.0 Kuhusu Matengenezo ya barabara:-

Mjumbe mmoja alieleza kuwa TARURA Wilaya iliingiza barabara za Kata ya Kihonda kwenye mfumo ili zitengenezwe lakini kwa sasa wanasema hazipo. Mjumbe alieleza kuwa kwa kuwa Serikali iliruhusu Halmashauri kuweza kuzichonga barabara kwa dharura, alipendekeza kuwa utekelezaji ufanyike ili kuondoa kero ya ubovu wa barabara za Manispaa

Jibu

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imetenga kwenye bajeti yake ya mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi cha **Tshs. 200,000,000.00** kwa ajili ya kuchonga barabara za Manispaa, utekelezaji utaanza mwezi Julai 2022. Aidha, Halmashauri imetenga kiasi cha **Tshs. 400,000,000.00** kwa ajili ya kuchonga barabara na kuzifungua kisha kukabidhiwa TARURA. Vilevile Halmashauri ina mpango wa kununua greda hivyo kero hiyo itatatuliwa.

2.0 Kuhusu umaliziaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya SINA Kata ya Mafisa:-

Mjumbe alitaka kujua ni lini Halmashauri itatekeleza ahadi ya upelekaji wa fedha za umaliziaji ujenzi katika Kituo cha Afya SINA Kata ya Mafisa.

Jibu

Mkurugenzi wa Manispaa alieleza kuwa katika bajeti ya Halmashauri ya mwaka wa fedha 2021/2022 zimetengwa fedha kwa ajili ya umaliziaji wa Kituo cha Afya SINA lakini Wizara ya Afya ilikataza umaliaji huo na badala yake ilielekeza ijengwe Zahanati ya Tungi.

Aidha, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri imeendelea kutenga fedha za umaliziaji wa Kituo cha Afya SINA na utekelezaji utaanza mwezi Julai, 2022.

3.0 Kuhusu kutokukamilika kwa upimaji katika Mtaa wa Kilimahewa Kata ya Kiwanja cha Ndege.

Ilitolewa hoja kuwa ulifanyika upimaji katika Mtaa wa Kilimahewa Kata ya Kiwanja cha Ndege lakini haukukamilika, Mjumbe alitaka kujua ni lini upimaji utakamilika ili Wananchi waweze kumilikishwa viwanja.

Jibu

Ilifafanuliwa kuwa ni kweli kulikuwa na zoezi la urasimishaji mwaka 2017, upimaji ulifanyika lakini Mkoa haukupitisha michoro kwa madai kuwa eneo ni la matumizi ya viwanda na Wananchi waliojenga walivamia. Kwa sasa Serikali imefuta matumizi ya viwanda na taratibu za urasimishaji zinaendelea na taarifa itapelekwa katika Kamati ya Mipangomiji na Mazingira.

4.0 Kuhusu Kata ya Kauzeni kutokupatiwa pikipiki iliyoahidiwa na Halmashauri:-

Mjumbe alieleza kuwa Kata ya Kauzeni iliahidiwa kupatiwa pikipiki na Halmashauri lakini haijatekelezwa. Mjumbe alitaka kujua ni lini ahadi itatekelezwa.

Jibu

Ilielezwa kuwa Halmashauri imetenga fedha za kununua pikipiki kwenye bajeti yake ya mwaka 2022/2023 kwa ajili ya Watendaji wa Kata na Maafisa Ugani wa Kilimo hivyo utekelezaji utafanyika kuanzia mwezi Julai, 2022.

5.0 Kuhusu adha ya Wanafunzi wa shule ya Msingi za Manispaa kukaa chini.

Mjumbe mwingine alieleza kuwa shule za Msingi za Manispaa zinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa samani kama vile madawati na viti hivyo baadhi ya Wanafunzi kulazimika kukaa chini, Mjumbe alitaka kujua ni lini adha hiyo itatatuliwa na kwa kuzingatia Manispaa ilikata miti ya kutengenezea madawati hivyo yamepelekwa wapi?

Ufafanuzi

Mkurugenzi wa Manispaa alifafanua kuwa shule za msingi za Halmashauri zinakabiliana na Changamoto nyingi ikiwemo uchakavu wa Miundombinu yake kama vile majengo na vyoo na upungufu wa madawati hivyo Halmashauri haiwezi kuitatua na kuimaliza. Waheshimiwa Madiwani walishauriwa kuwa wakahamasishe Wananchi kupitia Mabaraza ya Maendeleo ya Kata ili wachangie baada ya kupata kibali kutoka kwa Mkuu wa Wilaya.

6.0 Kuhusu kutatuliwa mgogoro wa Ardhi katika Kata ya Lukobe.

Mjumbe mmoja alitaka kujua ni lini Wataalam wataenda kupima ardhi ya hekari **146** ambazo imeachiwa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) baada ya kushinda mgogoro uliokuwepo.

Jibu:

Mkurugenzi wa Manispaa alianza kwa kumpongeza Mkuu wa Wilaya ya Morogoro kwa kutatua mgogoro wa ardhi katika Kata ya Lukobe. Alieleza kuwa kwa sasa Manispaa inaendelea na zoezi la upimaji ardhi kwenye eneo la Kiegea **A** na **B** kwa kutumia vifaa vyake.

Aidha upimaji huo utakapokamilika vifaa na Wataalamu watahamia kwenye Kata ya Lukobe.

7.0 Kuhusu kuanzishwa Timu ya mpira wa miguu ya Manispaa Morogoro.

Mjumbe alitaka kujua ni lini Halmashauri itaanzisha Timu yake ya mpira wa miguu.

Jibu

Ilielezwa kuwa Halmashauri kwa sasa inaendelea kushirikiana na Wataalam wa mpira wa miguu ili kuendeleza mchezo huo. Aidha, Menejimenti imechukua pendekezo la kuanzisha Timu yake kwa ajili ya kulifanyia kazi.

8.0 Kuhusu shule ya Msingi Kiegea iliyopo Kata ya Kihonda

Mjumbe alitaka kujua ni lini shule ya msingi Kiegea itapata ruzuku ya uendeshaji wa shule ili Wanafunzi wasilipe ada.

Jibu

Ilielezwa kuwa kuanzia Mwezi Julai 2022 shule itapelekewa fedha za ruzuku.

9.0 Kuhusu zoezi la Anuani za makazi katika Kata ya Bigwa

Mjumbe alitoa hoja kuwa wapo watu hawakupewa mafunzo/ semina lakini walipewa kazi ya kuandikisha Anwani za makazi. Aidha Kata ya Bigwa zoezi halikufanyika kwa **asilimia 100** kwa kuwa zipo nyumba hazikufikiwa hivyo alitaka kujua ni lini zoezi litatekelezwa tena.

Jibu
Mkurugenzi wa Manispaa aliomba Waheshimiwa Madiwani wawe Wajumbe wa kutambua maeneo ambayo awali hayakufikiwa na watoe taarifa Manispaa ili yafikiwe, hivyo Mjumbe alijulishwa kuwa litatekelezwa.

10.0 Kuhusu kujenga mabweni kwenye shule ya Sekondari Mafiga
Mjumbe alitaka kujua ni lini shule ya Sekondari Mafiga yatajengwa mabweni ya kulala wanafunzi

Jibu
Mkurugenzi wa Manispaa alianza kwa kumpongeza Diwani wa Kata kwa kusimamia elimu. Aidha, alieleza kuwa changamoto iliyopo ni ufinyu wa ardhi hivyo inahitaji kuomba ardhi kutoka SUA.

11.0 Kuhusu mpango wa kuwaweka kambini Wanafunzi
Ilielezwa kuwa shule ya Kilakala ilikuwa na mpango wa kuwaweka Wanafunzi kambini. Mjumbe alitaka kujua utekelezaji utaanza lini.

Ufafanuzi:-
Ilielezwa kuwa kwa sasa Halmashauri haina fedha za kutekeleza mpango huo.

12.0 Kuhusu chakula Mashuleni
Mjumbe alitaka kujua ni lini Halmashauri itachangia fedha za chakula shuleni kwa kuzingatia kuwa Wananchi hawana fedha.

Jibu
Kwa sasa Halmashauri haina fedha za kuchangia chakula cha Wanafunzi shuleni. Aidha, Halmashauri ilishaelekeza wazazi na Wananchi wachangie suala hilo hivyo Mkurugenzi alisisitiza Waheshimiwa Madiwani walisimamie

13.0 Kuhusu mitihani ya kujipima ya ndani na nje
Mjumbe alipendekeza Manispaa iandae mitihani ya kujipima ya ndani na nje ili kusaidia ufaulu kwa Wanafunzi.

Jibu
Ilielezwa kuwa Manispaa inaendelea kuandaa mitihani ya kuwapima Wanafunzi ili kujiandaa kufanya mitihani ya Taifa ya kidato cha Sita itakayofanyika mwezi Mei, 2022.

HMM/BM/84/ 2021/2022 Kusoma kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani ya Tarehe 01/02/2022 (Taarifa za Kata), Tarehe 03/02/2022 (kawaida), tarehe 10/02/2022 (Mapitio ya bajeti 2020/2021), Tarehe 10/02/2022 (Uwasilishwaji wa Bajeti ya mwaka 2022/2023) na Tarehe 10/02/2022 (Bajeti ya TARURA).

Mihtasari haikuwa na masahihisho hivyo ilithibitishwa kwa kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbukumbu sahihi za mikutano.

HMM/BM/85/ 2021/2022 Yatokanayo na mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 03/02/2022 (kawaida) na tarehe 10/02/2022 (maalum bajeti).

1.0 Kuhusu kuongezeka kwa madanguro kwenye eneo la Manispaa:-

Azimio

Kwa kuwa ziara haikufanyika mwezi Januari 2022, Baraza la Madiwani liliagiza Menejimenti kuandaa ziara hiyo mwezi Februari 2022 ili Kamati ikatoe elimu kwa jamii kuhusu kuacha kujihusisha na vitendo vya ngono zembe.

Utekelezaji

Agizo limetekelezwa, ziara ilifanyika tarehe 14/04/2022 katika maeneo ya hoteli ya Star Park na Samaki Samaki.

Mjadala na maagizo:-

Ilielezwa kuwa ziara ilifanyika katika kipindi cha mfungo hivyo hali halisi haikuweza kuonekana, hivyo ilishauriwa ziara hiyo irudiwe tena. Mkurugenzi wa Manispaa alichukuwa ushauri huo kwa utekelezaji.

2.0 Kuhusu ukusanyaji wa kodi ya huduma (service levy).

Azimio

Mkuu wa Wilaya alitoa muda wa siku saba (7) kuanzia tarehe 10/2/2022 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kukusanya kodi ya huduma (service levy) kwenye vituo vya kuuzia mafuta, watakaokaidi kulipa vituo vyao vifungwe.

Utekelezaji

Agizo limezingatiwa. Vituo vinne vilipelekewa notisi ambapo Oryx, Mwananchi na TSN walilipa isipokuwa POLLOT Investment na GAPCO.

Mjadala

Wajumbe walitaka kujua hatua gani zimechukuliwa dhidi ya waliokaidi kulipa kodi ya huduma. Aidha, Wafanyabiashara wengine wafuatiliwe ili walipe mapato.

Ufafanuzi

Ilielezwa kuwa ofisi ya Mkoa ilitoa maelekezo kwa wadaiwa wote walipe mapato wanayodaiwa. Aidha orodha ya Wafanyabiashara wengine ilipelekwa kwa Mkuu wa Mkoa ili aipitie kisha ashushe kwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro kwa utekelezaji. Tayari baadhi yao kama Kampuni ya Kajenjere tarehe 28/04/2022 ililipa kodi ya huduma **Tshs. 100,000,000.00.**

3.0 Kuhusu wauza mbogamboga na matunda katikati ya mji:-

Azimio

Kila Mheshimiwa Diwani apewe nakala ya mchoro wa mabanda ya Wafanyabiashara Ndogondogo (machinga) mkabala na eneo la Zimamoto ili waifahamu.

Utekelezaji

Agizo limetekelezwa. Nakala ya michoro ya mabanda walipewa Wajumbe.

Mjadala na Maagizo

Baraza lilipongeza ujenzi uliofanyika. Mjumbe alitaka kujua ni lini soko la Wafanyabiashara ndogondogo eneo la Zimamoto litakamilika na lini Wafanyabiashara wataanza kufanya biashara pia mchanganuo wa matumizi ya fedha **Tshs. 200,000,000.00** utapelekwa kwa Wajumbe.

Ufafanuzi

Ilielezwa kuwa ujenzi wa soko umefikia asilimia 95, meza zipo kwa sasa Menejimenti inaendelea kujenga vyoo na ilipendekezwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro awe mgeni rasmi kulifungua.

Agizo

Menejimenti iwasilishe mchanganuo wa fedha **TShs 200,000,000.00** za ujenzi wa mabanda ya Wafanyabiashara ndogo ndogo eneo la Zimamoto kwenye kikao kijacho cha Kamati ya Fedha na Uongozi kisha kwenye mkutano ujao wa Baraza la Madiwani.

4.0 Kuhusu eneo la shule ya Msingi Kiwanja cha Ndege Manispaa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Azimio

Halmashauri ifanye uchunguzi ili kubaini eneo la shule, Manispaa Jeshi la Zimamoto na eneo la wazi.

Utekelezaji

Agizo limezingatiwa. Uhakiki umefanyika na mipaka yote imewekwa. Aidha, shughuli mbalimbali zinazofanyika ndani ya eneo la Shule, Zimamoto na barabarani zimetambuliwa ikiwa ni pamoja na wahusika wanaoendesha shughuli hizo za biashara na sehemu wanapolipa kodi. Taarifa iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya kwa hatua zake zaidi.

HMM/BM/86/2021/2022 Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo

1.0 Kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi aliwasilisha taarifa hiyo. Wajumbe waliipokea na kuiridhia.

Mjadala na maagizo

Kuhusu sheria inayomtaka Mwananchi kulipia kibali cha ujenzi kwa nyumba zilizokwisha jengwa ndipo aunganishiwe maji na Mamlaka ya Maji MORUWASA.

Agizo

Baraza la Madiwani lilimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa kuiandikia barua Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro (MORUWASA) ili iache kudai vibali vya ujenzi kwa nyumba zilizokwisha jengwa kuanzia mwaka 2015 kurudi nyuma.

Kuhusu mapato ya Viosk:-
Baraza liliipongeza Kamati ya Fedha na Uongozi kwa kufuatilia mapato ya Viosk vilivyopo jirani na Market View.

Baraza lilielekeza kuwa vioski vipo katika maeneo mengi kama vile SIDO kwa hivyo zoezi hilo liwe endelevu kwenye maeneo yote na watakaokutwa wapewe mikataba kama ilivyofanyika katika Mtaa wa Kitope Road.

Mwenyekiti alipokea taarifa hiyo na kuomba Kamati ipewe ushirikiano pindi itakapopita kufuatilia mapato hayo.

Baada ya mjadala, Wajumbe waliiridhia taarifa.

2.0 Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022
Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa na Wajumbe waliipokea kisha Baraza iliiridhia

3.0 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022.
Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa na Wajumbe waliipokea kisha Baraza iliiridhia.

4.0 Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022.
Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa na Wajumbe waliipokea kisha Baraza iliiridhia

Aidha, Baraza liliamua kuwa taarifa ya Kamati ya Maadili ya Madiwani itajadiliwa pindi Baraza la Madiwani litakapojigeuza kama Kamati.

HMM/BM/87/2021/2022 Mapitio ya Sheria Ndogo ya ada ya uzoaji wa taka ya mwaka 2019

(A) Mapitio ya Sheria Ndogo ya ada ya uzoaji wa taka ya mwaka 2019:-
Menejimenti iliwasilisha mapitio ya Sheria Ndogo ya ada ya uzoaji taka ya mwaka 2019.

Ilielezwa kuwa sababu ya kufanya marekebisho hayo ni kutokana na viwango vilivyokuwepo awali kutokukidhi gharama za kuuweka mji katika

pamoja na mapendekezo ya sheria ndogo ya usafi wa mazingira za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro za mwaka 2022.

hali ya usafi wakati wote na kuondoa malalamiko ya kucheleweshe kuondoa taka kwa wakati.

Mapendekezo

Menejimenti ilipendekeza kama ifuatavyo:-

i) Ada ya uzoaji wa taka kwa Kaya inayotozwa kwa mwezi ya **Tshs. 1,000.00** iwe inatozwa kwa nyumba yenye familia moja **Tshs. 3,000.00** kwa mwezi.

ii) Nyumba yenye wapangaji kila mmoja atoe **Tshs. 1,000.00** kwa mwezi

iii) Maeneo ya biashara ada zake zibaki kama zilivyokuwa kwenye Sheria Ndogo za ada na ushuru ya mwaka 2019 kwani zinakidhi gharama za uondoaji taka kila siku katika maeneo hayo.

Maamuzi

Baraza la Madiwani liliridhia marekebisho ya Sheria Ndogo ya ada ya uzoaji taka ya mwaka 2019.

(B) Mapendekezo ya Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ya mwaka 2022.

Menejimenti iliwasilisha Mapendekezo ya Sheria Ndogo hiyo na ilipokelewa.

Mjadala

Wajumbe walieleza kuwa Kampuni ya Usafi wa Mazingira ya Kajenjere iongeze kasi ya kuzoa taka kwenye Mitaa kwa kuongeza tripu kwa Siku. Aidha, kuna malalamiko kutoka kwa Wananchi kuwa Kampuni ya Kajenjere inabeba viroba vikubwa vya kuhifadhi taka hivyo waache kufanya hivyo. Wajumbe pia walishauri kuwa kuwepo na daftari pindi Mwananchi anapozolewa taka asaini ili ijulikane kwa Mwezi amezolewa mara ngapi.

Kuhusu soko la Mawenzi kutokuzolewa Taka kwa muda mrefu

Ilielezwa kuwa soko la Mawenzi taka hazijazolewa kwa muda mrefu. Baraza lilijulishwa kuwa Kampuni ya Kajenjere itafuatiliwa ili ikazoe taka hizo Sokoni hapo.

Kuhusu Kata ya Tungi kutokuzolewa taka tangu Mwezi Novemba, 2021.

Mjumbe aliwasilisha hoja kuwa Kata ya Tungi haijazolewa taka tangu mwezi Novemba, 2021 hivyo alitaka kujua hatua gani zimechukuliwa.

Mkurugenzi wa Manispaa alieleza kuwa atalifuatilia suala hilo na aliahidi ndani ya muda wa siku mbili kuanzia tarehe 29/4/2022 taka zitazolewa.

Baraza lilipendekeza kuwa Halmashauri itangaze zabuni ya uzoaji taka ili apatikane Mzabuni wa kuzoa taka kwenye maeneo ambayo Kampuni ya Kajenjere imeshindwa kuyafikia.

Kuhusu vikundi kazi katika Kata ya Mindu

Mjumbe alishauri kuwa vikundi kazi vya kuzoa taka vitokane na wenyeji wa eneo husika.

Baada ya Mjadala, Baraza la Madiwani liliridhia mapendekezo ya Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ya Mwaka 2022 kwa hatua zaidi.

HMM/BM/88/2021/2022 Taarifa ya Muundo wa Mgawanyo wa Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM)

Mkurugenzi wa Manispaa aliwasilisha Taarifa ya Mgawanyo wa majukumu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama ilivyoidhinishwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 29 Januari 2022.

1. Mabadiliko na Muundo ulioidhinishwa na Serikali ni Kama ifuatavyo:-

i) Kufuta Idara ya Ujenzi na Zimamoto na kuanzisha Idara ya Miundombinu na Maendeleo ya Vijiji na Miji kutokana na majukumu ya Zimamoto kuhamishwa kutoka MSM kwenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hivyo Idara ya Miundombinu itatekeleza majukumu ya ujenzi, barabara ya kusimamia maendeleo ya Vijiji na Miji. Idara hii itakuwa na sehemu tatu (3) ambazo ni:-

- Sehemu ya Ujenzi
- Sehemu ya Barabara na
- Sehemu ya Maendeleo ya Vijiji na Miji

ii) Kubadili jina la Idara ya Afya kuwa Idara ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe ili kuakisi majukumu ya Ustawi wa Jamii na Lishe yanayotekelezwa na Idara hii. Idara hii itakuwa na sehemu tatu (3) ambazo ni

- Sehemu ya Huduma za Afya
- Sehemu ya Ustawi wa Jamii na
- Sehemu ya Huduma za Lishe.

Aidha inapendekeza kubadili jina la Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya vijana kuwa Idara ya Maendeleo ya Jamii

iii) Kuhamisha jukumu la biashara kutoka Idara ya Fedha na Biashara kwenda Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili kuimarisha uratibu wa majukumu yanayoshabihiana.

Aidha, Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itakuwa na Sehemu mbili (2) Zifuatazo:-

- Sehemu ya Maendeleo ya Viwanda na Uwekezaji na
- Sehemu ya Biashara na Masoko

Aidha, ilipendekezwa kuanzisha Kitengo cha Fedha na Uhasibu ili kuongeza ufanisi.

iv) Kuongeza jukumu la elimu maalum, elimu ya Watu wazima na elimu isiyo rasmi chini ya Idara ya Elimu Msingi na kubadili jina la Idara ya Elimu ya Awali na Eimu Msingi ili kuimarisha usimamizi na uratibu. Idara hii itakuwa na sehemu nne (4) zifuatazo:-

- Sehemu ya Taaluma
- Sehemu ya Takwimu na Logistiki
- Sehemu ya Elimu Maalum na
- Sehemu ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu isiyo Rasmi

v) Kuongeza jukumu la elimu maalum, elimu ya watu wazima na elimu isiyo rasmi chini ya Idara ya Elimu ya Sekondari ili kuimarisha usimamizi na uratibu. Idara hii itakuwa na sehemu nne (4) kama ifuatavyo:-

- Sehemu ya Taaluma
- Sehemu ya Takwimu na Logistiki
- Sehemu ya Elimu Maalum na
- Sehemu ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu isiyo rasmi.

vi) Kuunganisha Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika na Idara ya Mifugo na Uvuvi kuwa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kuwa majukumu yake yanaweza kutekelezwa pamoja na ufanisi zaidi. Idara hii itakuwa na sehemu tatu (3) kama ifuatavyo:-

- Sehemu ya Kilimo
- Sehemu ya Mifugo na
- Sehemu ya Uvuvi

vii) Kufuta Kitengo cha Uchaguzi kwa kuwa majukumu yake hutekelezwa na Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu.

viii) Kuhamishia jukumu la Takwimu kutoka Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwenye Kitengo cha TEHAMA ili kutekeleza maelekezo ya Serikali. Aidha, jina la Kitengo litabadilika kuwa Kitengo cha TEHAMA na Takwimu ili kuakisi kazi zitakazofanywa na Kitengo hiki.

Aidha, inapendekezwa kubadili jina la Idara ya Mipango, Takwimu na ufuatiliaji kuwa Idara ya Mipango na Uratibu yenye sehemu mbili (2) zifuatazo:-

- Sehemu ya Mipango na Bajeti na
- Sehemu ya Ufuatiliaji na Tathmini

ix) Kufuta Idara ya Maji na majukumu yake kutekelezwa na Ofisi za Wilaya ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Uratibu wa taarifa za Sekta ya Maji zitatekelezwa na Idara ya Mipango na Uratibu iliyopendekezwa.

x) Kuhamisha majukumu ya maendeleo ya Vijana kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Vijana na kuanzisha Kitengo cha Michezo, Utamaduni na Sanaa.

xi) Kubadili jina na hadhi ya Idara ya usafi na Mazingira kuwa Kitengo cha 'Waste Management and Sanitation' ili kuakisi kazi zitazofanywa na Kitengo. Aidha, jukumu la usimamizi wa mazingira litatekelezwa na Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi

xii) Kufuta Idara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ili kutekeleza maelekezo ya serikali ya kuhamisha uwajibikaji wa kiutumishi na kiutendaji kwa Watumishi wa Sekta ya Ardhi kutoka MSM kwenda Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, majukumu ya Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira yatatekelezwa na Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira.

xiii) Kufuta Kitengo cha Nyuki na majukumu yatekelezwe na Kitengo cha Maliasili na uhifadhi wa Mazingira zinazofanywa na Kitengo hiki.

xiv) Kuonesha Ofisi za Utendaji Kata (Ward Executive Office) na Ofisi za Utendaji Vijijini/Mtaani (Vilage/Mitaa Executive Office) katika muundo ili kuendana na viwango vya Miundo ya Taasisi za Umma.

xv) Kutumia neno 'Division' badala ya 'Department na Sehemu (Section) kwa ajili ya mgawanyo wa majukumu chini ya Idara;

xvi) Kubadili nafasi ya Mkuu wa Idara ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe kuwa "Council Medical Officer of Health" (CMoH) badala ya "District Medical Officer" (DMO) kwa kuwa Halmashauri zinatofautiana kulingana na hazi zao.

xvii) Majina ya Wakuu wa Sehemu kuwa 'Officer In Charge,

2. Kutokana na mabadiliko hayo, Muundo ulioidhinisha utakuwa na Idara na Vitengo kama ifuatavyo:-
   i) Idara ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijijini na Mijini
   ii) Idara ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe
   iii) Idara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji
   iv) Idara ya Elimu ya Awali na Msingi
   v) Idara ya Elimu ya Sekondari
   vi) Idara ya Maendeleo ya Jamii
   vii) Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi
   viii) Idara ya Mipango na Uratibu
   ix) Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu
   x) Kitengo cha 'Waste Management'
   xi) Kitengo cha Maliasili na Hifadhi ya Mazingira
   xii) Kitengo cha Michezo, Utamaduni na Sanaa
   xiii) Kitengo cha Fedha na Uhasibu
   xiv) Kitengo cha Huduma za Sheria
   xv) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
   xvi) Kitengo cha Usimamizi na Ununuzi
   xvii) Kitengo cha TEHAMA na Takwimu
   xviii) Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
   xix) Ofisi ya Mtendaji Kata
   xx) Ofisi ya Kijiji/Mtaa

3. Hivyo katika utekelezaji wa Muundo huo hatua zifuatazo zizingatiwe:-
   i) Kujaza Nafasi za uongozi zilizowazi kwenye Muundo ulioidhinishwa kulingana na Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma.

   ii) Kuandaa mahitaji ya Watumishi (Job List) ambao watahitajika katika kutekeleza majukumu na kazi za Muundo huu mpya kulingana na Miundo ya Utumishi (Schemes of Service).

iii) Kuandaa maelezo ya kazi (Job Descriptions) kwa kila nafasi ya kazi katika Halmashauri.

iv) Kuwaelewesha Watumishi wote juu ya Muundo mpya ili kurahisisha utekelezaji wake.

v) Kuwasilisha Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora taarifa ya Utekelezaji wa Muundo na Mgawanyiko wa Majukumu ifikapo tarehe 05 Julai, 2022 Taarifa hiyo iwe na maelekezo ya nafasi za Uongozi zilizojazwa orodha ya Mahitaji ya Watumishi na Maelezo ya kazi kwa Watumishi wote.

Baraza lilipokea na kuiridhia taarifa hiyo.

HMM/BM/89/ 2021/2022 Taarifa mbalimbali.

A) Mapendekezo ya wafanyakazi hodari kwa Mwaka 2020/2022

Kabla ya kujadili Agenda hii Baraza lilijigeuza kama Kamati na Kanuni ya uendeshaji wa vikao vya siri vya Kamati zilizingatiwa.

Afisa Utumishi wa Manispaa aliwasilisha Mapendekezo ya Wafanyakazi hodari wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa Mwaka 2022 ambayo pia yaliridhiwa na Kamati ya Fedha na Uongozi kwenye kikao chake cha tarehe 21/4/2022.

Maamuzi ya Baraza la Madiwani

Baraza la Madiwani liliridhia majina yaliyopendekezwa, wawe Wafanyakazi hodari kwa mwaka 2021.

B) Taarifa ya mashauri ya nidhamu ya Watumishi tisa (9) wa kada mbalimbali.

Afisa Utumishi wa Manispaa aliwasilisha taarifa ya mashauri ya nidhamu kwa Watumishi tisa (9) wa kada mbalimbali kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi 2022 kwa ajili ya kutolea maamuzi ya Baraza.

Maamuzi

Baraza la Madiwani liliamua kuwasamehe Watumishi wote waliokuwa na mashauri ya nidhamu kwa kipindi cha robo ya tatu (Januari – Machi, 2022) na kuelekeza kuwa wasipewe adhabu yoyote.

C) Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Madiwani.

Taarifa iliwasilishwa na ilipokelewa.

D) Kuhusu Stendi ya Daladala Mafiga

Wajumbe walishauri na kuelekeza kuwa Mkuu wa Wilaya afanye kazi kwa ushirikiano na Baraza la Madiwani kupitia Kamati za Kudumu ili wawe na ufahamu kwa kila kinachofanyika katika Halmashauri.

Baada ya mjadala Baraza liliamua yafuatayo:-

Agizo

Baraza lilimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa, Wataalamu wa Manispaa na SUA waende katika stendi ya Daladala Mafiga kuangalia kama kilichofanyika pale kina tija kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na SUA na awasilishe taarifa kwenye Mkutano maalumu wa Baraza la Madiwani.

HMM/BM/90/ 2021/2022 Kufunga Mkutano

1. Baraza lilimpongeza Mhe, Abdulazizi Mohamed Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini kwa kutetea haki na maslahi ya Waheshimiwa Madiwani Bungeni. Baraza liliwaomba Mkurugenzi wa Manispaa na Mstahiki Meya wamfikishie pongezi hizo.

2. Naibu Meya aliwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Madiwani kwa kujitokeza katika mazishi ya Ndg Charles William Tunge Katibu wa CCM Kata ya Sabasaba yaliyofanyika tarehe 27/4/2022. Aidha, alimpongeza Mhe, Abdulazizi Mohamed (Mb) kwa kusaidia msiba huo.

3. Mstahiki Meya aliagiza kuwa Viongozi wa Manispaa wasimamie mara moja magari yanayoenda Wilayani kuanzia safari zao katika Stendi ya Mafiga na Stendi ya Mabasi Msamvu ni kwa ajili ya Mabasi yanayoenda Mikoani.

   Baada ya kusema hayo Mstahiki meya alifunga Mkutano Saa 11:22 Jioni.

Muhtasari umethibitishwa tarehe ……..……

……	……
Mhe. Pascal M. Kihanga	Ndg. Ally H. Machela
MSTAHIKI MEYA	MKURUGENZI WA MANISPAA
MWENYEKITI	**KATIBU**

YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 28/04/2022

MUHT. NA	AZIMIO	MTEKELEZAJI	UTEKELEZAJI
HMM/BM/81/ 2021/2022 Kufungua Mkutano	**1.0 Kuhusu mikataba ya Wafanyabiashara eneo la Zimamoto** Mkuu wa Wilaya aliagiza kuwa mikataba **51** ya Wafanyabiashara eneo la Zimamoto ambayo haipo rasmi ifutwe na kuingiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na kulipa Mapato ya Halmashauri.	Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi	Agizo limezingatiwa. Kikao kilimekaa tarehe 08/08/2022 Wajumbe wachache waliohudhuria watano, hawakuwa tayari kusaini mikataba hivyo Menejimenti imepanga kukaa tena kikao tarehe 14/08/2022 ili wakutane na wafanyabiashara wote.
	2.0 Kuhusu stendi ya Daladala Mafiga Mkuu wa Wilaya aliagiza kuwa Stendi ya Daladala Mafiga ifanye kazi, magari yote yanayoenda Wilayani yaanzie hapo.	Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya	Agizo limezingatiwa. Jumla ya magari 86 yanayotoa huduma za usafiri Morogoro yameainishwa. Aidha taratibu za mawasilino na mamlaka nyingine zinaendelea.
	3.0 Kuhusu wauza mbogamboga na matunda katikati ya mji Menejimenti iwasilishe mchanganuo wa fedha **Shs 200,000,000.00** za ujenzi wa mabanda ya Wafanyabiashara ndogo ndogo eneo la Zimamoto wenye kikao kijacho cha Kamati ya Fedha na Uongozi kisha kwenye mkutano ujao wa Baraza la Madiwani.	Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi	Agizo limezingatiwa. Taarifa ya mchanganuo wa matumizi ya fedha na ujenzi wa mabanda imeambatishwa kiambatisho …….. uk …….

HMM/BM/86/ 2021/2022 Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo	**4.0**	**Kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2021/2022.** Baraza la Madiwani lilimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa kuiandikia barua Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro (MORUWASA) ili iache kudai vibali vya ujenzi kwa nyumba zilizokwishajengwa kuanzia mwaka 2015 kurudi nyuma.	Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya.	Agizo limezingatiwa. Mkurugenzi Mtendaji MORUWASA aliandikiwa barua yenye Kumb. Na. ME/MMC-190/96 ya tarehe 23/05/2022 kumjulisha aache kudai vibali vya ujenzi kwa nyumba zilizokwishajengwa kuanzia mwaka 2015 kurudi nyuma. Angalia kiambatisho …….. uk ……..
HMM/BM/89/ 2021/2022 Taarifa mbalimbali	**5.0**	**Kuhusu Stendi ya Daladala Mafiga** Baraza lilimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa, Wataalamu wa Manispaa na SUA waende katika stendi ya Daladala Mafiga kuangalia kama kilichofanyika pale kina tija kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na SUA na awasilishe taarifa kwenye Mkutano maalumu wa Baraza la Madiwani.	Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi	Agizo limezingatiwa. Wabia wa mradi wa stendi ya Mafiga na SUA timu imekaa na kuwasilisha taarifa kwenye mkutano maalum wa Baraza la Madiwani la tarehe 28/06/2022. Taarifa ya tathmini ya mapato kwa eneo kutumika kama mnada kwa muda, imeambatanishwa kwa rejea. Angalia kiambatisho …….. uk ……..